

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFUJI



MKOA WA PWANI:
SIMU: 023 -2010304
Fax 023 - 2010317
Email: ded.rufiji@pwani.go.tz

S. L.P 28,
UTETE/RUFUJI.

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (MARUDIO) TAREHE 05/10/2017

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kupitia Nafasi **535** zilizotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais **TAMISEMI** kwa Kibali Kumb. Na. **AH.161/164/02/37** cha tarehe **21/06/2017**. Inawatangazia kuwepo kwa Nafasi **3** za Wasaidizi wa Hesabu DRJ II (Accounts Assistant II), watakaofanya kazi katika Kituo cha Afya **Mohoro, Ikwiriri** na **Nyaminywili**. Lengo kuu ikiwa ni kuimarisha usimamizi wa fedha katika vituo vya Afya.

Masharti ya Kibali

1. Wenye sifa tu ndio waombe
2. Ajira zao zitakuwa za Mkatoba wa Mwaka mmoja mmoja.
3. Mkatoba ukimalizika, Watumishi hawa hawataingizwa moja kwa moja katika utaratibu wa ajira za Serikali bali itategemea ufanisi na utendaji kazi wao.
4. Mishahara yao itanzia ngazi ya **TGS B** kima cha kuanzia ni shilingi **390,000/=**.

Sifa za Mwombaji:

1. Awe na cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali au cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

Kazi za Kufanya (Majukumu)

1. Kuandika na kutunza regista zinazohusu shughuli za uhasibu.
2. Kutunza kumbukumbu za hesabu
3. Kupeleka barua au nyaraka za uhasibu benki, ukusanyaji wa mapato
4. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkurugenzi Mtendaji (W) Rufiji.

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W) Rufiji,
S.L.P. 28,
UTETE/RUFUJI.

Maombi yanapokelewa kuanzia tarehe 05/10/2017 hadi tarehe 13/10/2017.

NB: Vitu vya kuzingatia; nakala ya cheti halisi cha kidato cha IV au VI, Taaluma, cheti cha kuzaliwa, CV (Taarifa binafsi) na picha mbili (passport size). Nakala za Vyeti vithibitishwe na Mahakama. Mtu yeyote atakayewasilisha nakala za matokeo (Result slips au Progressive results) hatafikiliwa katika maombi yake.

Rashidi S. Salum
Mkurugenzi Mtendaji (W)
RUFUJI